

Kohozi la kulazimishwa

Kuchukua sampuli kama sehemu moja wapo ya uchuguzi wa kifua kikuu

SWAHILI

Ukweli kuhusu kifua kikuu

Kifua kikuu ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria ya kifua kikuu (M. Tuberculosis). Bakteria hiyo husambaa kupitia kwa hewa kwa matone madogo wakati mtu aliye na kifua kikuu anapokohoa, toa chavia, ongea ama anapocheka.

Watu ambao wanapumua hewa hili wanaweza pumua ndani bakteria ile na waambukizwe. Takriban asilimia 10 ya watu wanaoambukizwa huugua kifua kikuu wakati mmoja maisha mwao. Kuhakikisha kana kwamba kuna ugonjwa wa kifua kikuu, lazima ufanye vipimo kadhaa. Kohozi la kulazimishwa ni moja wapo.

Kipimo hicho cha fanywa vipi? Wakati wa kipimo utapumua ndani maji ya chumvi kupitia kwa kifaa cha kufanya mvuke kilicho unganishwa na oksigeni. Ukungu utakaotokana na hapo utachangamua njia za hewa ndiposa iwe rahisi kukohoa kikohozi kutoka kwa mapafu.

Matayarisho Usile wala unywe chochote kwa masaa 4 kabla ya kipimo

Kifua kikuu chaambukizwa vipi?



Hadi kwa mpokezi anayepumua ndani matone yaliyo na bakteria ya mapafu.



Kutoka kwa mtu aliye na kifua kikuu cha mapafu aliye na tubercle basillus kwenye kikohozi.



Uma kidomo na ushikilie midomo yako pale kwa nguvu. Pumua ndani na nje kwa kawaida kupitia mdomo wako. Pumua punzi nzito mara kwa mara. Maji (ukungu ukisha shikamana) yatakayopatikana humezwa



Utakapohisi kukohoa, toa nje kifaa cha kufanya mvuke na ukohoe kwa nguvu mara kadhaa.



Tema makamasi yote utakayokohoa kutoka kwa mapafu moja kwa moja ndani ya glasi ya kipimo. Kuzuia kuchafua glasi ya kipimo, glasi hiyo hushikiliwa chini ya mdomo wa chini.

Lazima urudie utaratibu huo mara kadhaa. Fuata maelezo uliyopewa. Funika kifuniko kipimo kinapokamilika. Mwishowe, osha mikono yako.

Ni nini kifuatacho?

Matokeo ya vipimo itakuwa tayari baada ya wiki 6 hadi 8. Utaitwa kwa mkutano. Kulingana na matokeo ya vipimo, daktari ataamua nini kifuatacho.